**LBE Komputa na Intaneti – Programme 8**

Mwandishi : Richard Lough

Muhariri : Maja Dreyer

Tafsiri: Eric Ponda

| |
|---|
| **Wahusika:** Beatrice (Msichana wa makamu l), John (Mvulana wa makamu), Komputa er (Sauti)<br>**Kitiwa sauti:** Clement Mwange (mfasiri, miaka 30)<br>**Sauti nyingine** kutoka Studio. |

**Package 8.1**

**Muziki – [Full up for 0.10 then fade under Intro]**

**Intro:**

Hujambo na karibu tena msikilizaji kwa makala nyingine ya Noa Bongo Jenga Maisha yako tukizungumzia Komputa na Intaneti. Katika kipindi cha leo, Beatrice na John wanajifunza jinsi ya kutumia kompyuta kushiriki masuala ya siasa. Yaani, jinsi Komputa inavyoweza kukupa habari muhimu kuhusu maendeleo ya kisiasa barani Africa, na ulimwengu mzima kwa jumla. Huku mataifa mengi yakijaribu kubana habari kwa raia wake, mtandao wa Intaneti unaweza kuwasaidia watu kujifunza vile mataifa yao yanavyochukuliwa machoni mwa ulimwengu na zaidi kuhusu yale yanayoendelea nchini mwao.

**Package 8.1**

**SFX_Dialing_Up_Internet [Fade under…]**

**1. Computer:** Habari John, habari Beatrice…

**2. Beatrice:** Habari Komputa . Nimepokea Email kutoka kwa rafiki yangu wa kike anayeishi nchini Sudan ambaye tumekuwa tukiwasiliana moja kwa moja kupitia mtandao. Anasema kuwa kuna kurasa nyingi anazotumia kujifahamisha na yale yanayotendeka nchini mwake kwani anasema habari zinazotolewa na serikali si za kuaminika.

**3. Kompota:** Hebu kidogo nijiunganishe na mtandao, lakini anayosema rafiki yako nchini Sudani ni kweli, na mambo la kufurahisha. Yako mataifa mengi ulimwenguni hasa barani Africa ambako serikali nyingi zinabana habari muhimu kwa raia wake.

**4. John:** Kweli ? Kwa hivyo hatupasi kuamini kila kitu kinachosemwa na serikali?

| | |
|---|---|
| **5. Komputa :** | Nadhani ni jambo la busara kuthibitisha kwanza habari zinazotolewa na viongozi wa kisiasa na serikali kote ulimwenguni.. Lakini yapo mashirika mengi tu yanayoweza kutusaidia kufahamu vyema ukweli wa mambo au kuthibitisha habari hizi. |
| **6. Beatrice:** | Ndio, hivyo ndivyo anavyomaanisha rafiki yako kutoka Sudan. Kwa mfano anasema kuwa huwa anangalia kurasa nyingi zenye habari kuhusu haki za binadamu na shirika la Amensty International kujua nini kinachoendelea nchini mwake. |

**SFX_Akiandika kwa Komputa.**

| | |
|---|---|
| **7. John:** | Ni mashirika gani mengine yanayotajwa na rafiki yako Beatrice? |
| **8. Beatrice:** | Pia anasema kuwa naweza kuangalia katika ukurasa wa Jumuiya ya Africa, na vile vile Umoja wa mataifa ambayo hutoa msimamo wake kuhusu hali ilivyo katika mataifa yanayokumbwa na mizozo. |

**9. John:** Je, kuhusu Kenya kwa mfano (au taifa jingine.) ambalo lina serikali ya umoja wa taifa, nataka kufanya utafiti kuhusu muungano huo unavyofanya kazi. Je, serikali zina kurasa za tovuti kwenye mtandao?

**10. Komputa:** Ndio karibu serikali nyingi zina kurasa za tovuti katika mtandao. Kwa mfano, iwapo unataka kujua ni nani anayesimamia wizara Fulani, naweza kwanda kwa ukurasa wa mtandao wake. Au labda unataka kujua kuhusu masuala ya katiba, na vipi inavyokuathiri wewe,familia yako na marafiki,unaweza kutembelea mtandao ambao utakujuza zaidi.

**11. John:** Sikudhani kuwa serikali pia zinaweza kuwa na kurasa za tovuti, nilifikiri ni asasi za kibiashara na mashirika mengine ya kawaida.

**12. Komputa:** Jambo moja la kusitiza hapa John na Beatrice , ni kwamba mashirika yote, ya kiserikali ,yasiyo ya kiserikali, yale ya kutetea haki za binadamu, yana ajenda zao yanazotaka kutimiza. Kwa hivyo si jambo la busara kuamini habari zote unazozisoma kwenya mtandao kuhusu mashirika haya.

**12. Beatrice:** Kwa hivyo mara nyingine yanatoa habari za uongo?

**13.Komputa:** Si wakati wote. Ninachomaanisha ni kwamba mashirika haya yanataka kuzingatia maslahi yao kama ilivyo kwa wengi wetu, na pia yanataka kuelezea msimamo wao kwa ulimwengu mzima. Kwa hivyo ni vizuri kuelewa na kuthibitisha habari unazozisoma kwenye mtandao, na hapo utafiti kupitia mtandao wa Intaneti huwa muhimu.

**14. John:** Unamaanisha nini?

**15.Komputa:** Hii ndio sababu mtando wa Intaneti huwa muhimu kwetu kwa masuala haya ya utafiti. Hukupa habari na maoni ya watu mbali mbali kukuwezesha wewe kufanya maamuzi ya busara.. Na hi ndio maana ya demokrasia na uhuru wa kutoa maoni!.

**16. Beatrice:** Ni vigumu kuelewa mambo yalivyokuwa kabla ya kuwasili kwa teknolojia hii ya Intaneti Kuna mengi sana ya kusoma na kujifunza.

**17. Komputa:** Inachemsha bongo lakini pia ni rasilimali na chombo muhimu. Hakikisha unakitumia vyema na kwa busara.

**18. John na Beatrice:** Asante Komputa busara yako!

**Music – [Full up for 0.10 then fade under ]**

**SFX_Mkahawa wa Java_ [Fade under…]**

**1. Beatrice**: John, kuna Mtu pale anayetumia mtandao wa intaneti. Huenda anatumia simu ya mkononi .

**2. John:** Ni kweli hebu twende!.

**3. Beatrice:** Habari, mimi na rafiki yangu John tunafanya utafiti kuhusu komputa na Intaneti, unaweza kutueleza kwanini umeamua kutumia simu yako ya mkononi! Ni ya kazini yako?

**Clip: 8.2_Clement_1**

Ninaitwa Clement Mwange,mimi ni mkalimali. Nimeamua kutumia simu yangu ya mkononi kwa sababu kazi yangu inanihitaji kutembea sehemu nyingi.

**4. Beatrice:** Mkalimali? Kumbe!.

**Clip: 8.2_Clement_2**

Nahitajika kuhudhuria vikao vingi wakati ninapofanya kazi zangu za ufasiri katika mahotelini ambako mara nyingi huwa vigumu kuunganishwa, na iwapo utapata bahati ya kuunganishwa, huwa gharama ya juu. Hii ndio sababu niliamua kutumia simu yangu ambayo naweza kuitumia hata nyumbani.

**5. John:** Lakini unawezaje kuunganishwa bila ya waya ambazo hutumiwa kuunganisha mtandao wa intaneti mikawani?

**Clip: 8.2_Clement_3**

Kuna njia mbili za kufanya hivyo. Ya kwanza unaweza kutumia simu yako ya mkononi kwa urahisi, kwa kuwa unatumia tu laini yako ya simu. Unachohitaji ni kuunganisha laini yako na mtandao wa Intaneti..

**6. Beatrice:** Lakini hii sio unayotumia, kwasababu simu yako haijaunganishwa na ***Laptop!***

**Clip: 8.2_Clement_4**

Ndio njia nyingine, unaweza kununua kiunganisho kinachofahamika kama ***USB modem*** ambacho ni rahisi kutumia. Nyingi yazo unaweza tu kuzingunisha na laini ya mtandao na nyngine unaweza kuziweka kwa komputa yako kwa kutumia ***CD ROM***

**7. John:** Clement, kwa hiyo hii imerahisha kazi yako ambapo unaweza kutuma *email* zako wakati wowote?

**Clip: 8.2_Clement_5**

Ndio, hii imenirahisishia kazi zangu kwasababu ninaishi nje ya jiji la Nairobi na kupata huduma nzuri ya mtandao wa Intaneti ni lazima nisafiri hadi jijini kila siku hata jumapili, na wakati mwengine hurudi nyumbani kuchelewa.

**8. John:** Pia sisi tunatatizika sana, tunaujuzi wa kutumia mtandao wa Intaneti,lakini hatuwezi kutumia ujuzi huu wakati wowote hadi tupate mahali kuna mkahawa wa Intaneti baada ya kutoka shule au mwishoni mwa wiki. Lazima uwe unafurahia huduma za kuwa na mtandao mahali popote uendapo!

**Clip: 8.2_Clement_6**

Ni kweli kwasababu huduma hizi zinanisaidia sana, wakati ninapokuwa na dharura naweza kufanya kazi mahali popote, ofisini, nyumbani , mkawahani ninapopata kikombe cha chai ,nikiwa kwenya gari langu , hata kwenye basi la abiria!.

**9. John:** Pia unatumia kwa shughuli zako nyingine mbali na kazi?

**Clip: 8.2_Clement_7**

Ndio, nawezakuitumia kwa shughuli nyingine za uraibu kama vile kufuatilia kandanda na mengineyo.

**10. John:** Niajabu:Unaweza kufuatialia kandanda masaa 24! Lakini je Clement, huduma zake ni za kuaminika au ni kama zile unazozipata katika baadhi ya mikahawa?

**Clip: 8.2_Clement_8**

Kwa bahati mbaya, bado tunatatizo la kasi ya kuunganishwa na intaneti hasa hapa nchini Kenya, kwasababu hatutumii uzi wa kuunganisha huduma hizi na sehemu nyingine za ulimwengu ambazo ni thabiti na za kuaminika. Tatizo jingine ni eneo, mara nyingi maeneo mengi hukumba na tatizo la kukatizwa au ukosefu wa huduma za mtandao. Lakini naweza kusema ni vyema kuwa na huduma hizi za mkononi..

**11. Beatrice:** Tayari imeanza kubadilisha maisha yako, sasa unataka kuwa katika mkahawa wa mtandao kila siku.!

**12. John:** Tunakuonea wivu Clement! Lakini tumeshukuru kwa maelezo yako kuhusu unavyoweza kutumia simu yako ya mkononi kuunganishwa na mtandao wa Intaneti. … Labda tutakapokuwa na ***Laptops*** zetu tutaweza kuunganishwa mahali popote wakati wowote. Siwezi kusubiri kupata ***Laptop*** hiyo!

**13. Beatrice:** Hata mimi pia litakuwa jambo la kufurahia. KwaheriClement!

**Outro:**

Na hadi kufikia hapo hatuna budi kutia nanga kwa leo. John na Beatrice wanaendelea kutafakari matumaini yao ya siku za usoni. Ungana nasi mara nyingine usikilize kipindi kingine kuhusu komputa na Intaneti. Ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki pamoja na rafiki zako unaweza kuitembelea tovuti yet: www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine Kwaheri..

**Mwisho**